

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

*Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni Idaraya Serikali inayojitegemea ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi hii imeanzishwa mara baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini kwa Sheria ya Vyama vya Siasa Suraya 258. Majukumuya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura ya 278 ambayo hutumika katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani.*

### **Wasiliana nasi**

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa  
Viwanja vya Nanenane Nzuguni  
Jengola Wizaraya Kazi - Mtaa wa Nzuguni A  
S.L.P 2851  
DODOMA

## VITENDO VINAVYOKATAZWA NA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA

### *Katika kipindi cha uchaguzi, chama cha siasa hakipaswi kufanyayafuatayo:-*

- (i) Kunadi sera zinazopingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Sheria zingine za nchi (Kifungu cha 6A(1));
- (ii) Kuunda kikundi cha ulinzi na usalama cha aina yoyote au kuwa na taasisi inayolenga kufanya majukumu ya Jeshi la Polisi au vikosi vingine vya ulinzi na usalama wa nchi (Kifungu cha 8E(1));
- (iii) Kuratibu, kuendesha au kufadhili mafunzo yoyote ya kutumia nguvu au silaha kwa wanachama wake au kwa mtu yeyote (Kifungu cha 8E(2));
- (iv) Kuhamasisha udini, ukabila na ukanda (Kifungu cha 9(2)(a));
- (v) Kuhamasisha kuvunjika kwa Muungano wa Tanzania au kuwa na lengo la kufanya siasa upande mmoja wa muungano (Kifungu cha 9(2)(b)(d));
- (vi) Kuruhusu au kuhamasisha matumizi ya nguvu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa (Kifungu cha 9(2)(c));
- (vii) Kuruhusu viongozi au wanachama wake kutumia maneno ya matusi, dhihaka, kashfa na uchochezi, yanayoweza kusababisha uvunjifu wa amani (Kifungu cha 9(2)(f));
- (viii) Kupeperusha bendera ya chama, kufanya siasa au kufungua tawi katika maeneo ya kazi, shule, vyuo, ibada, majengo ya Serikali au Umma (Kifungu cha 11C(3) na 12(2));
- (ix) Kutoa matamshi, kuandaa machapisho, kuharibu au kufanya kitendo chochote chenye dhamira ya kudhalilisha au kudhihaki bendera ya chama kingine (Kifungu cha 11C(5));
- (x) Kufanya mikutano au maandamano bila kufuata utaratibu wa kisheria (Kifungu cha 11).